**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI**

**Kumb. Na. AB.220/321/01E/82** **Tarehe: 10/11/2025**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni anawatangazia Watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Manispaa hii kuomba nafasi za kazi mbili (02) baada ya kupokea kibali kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao:-

### 1.0 DEREVA DARAJA LA II - NAFASI 2

### 1.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
ii. Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
vi. Kufanya usafi wa gari, na
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

### 1.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mwenye cheti cha kidato cha Nne (Form IV) na Leseni ya Daraja la “E” au “C” ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali na awe amehudhuria mafunzo ya Msingi ya uendeshaji Magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

**NGAZI YA MSHAHARA**

**TGS B**

**MASHARTI KWA UJUMLA KWA WAOMBAJI:**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.

ii. **Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuaninisha kwenye mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.**

iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza **(Detailed C.V**) yenye anuani inayotumika, namba ya simu za kuaminika, anuani ya barua pepe (E-mail Address) pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.

iv. Maombi yote yaambatane na Vyeti vya Elimu na Taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Mtihani wa Kidato cha IV au VI kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

v. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.

vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (**TCU, NECTA na NACTVET**) na taarifa ya uhakiki iambatishwe kwenye maombi.

vii. Testimonials, Provisional Results, Statement of results hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (form IV and form VI result slips) **HAVITAKUBALIWA.**

viii. Waombaji wa kazi ya Dereva Daraja II wenye leseni Daraja E au C wanapaswa **KUAMBATISHA** vyeti vya udereva vilivyo wapatia sifa ya kupata madaraja husika.

ix. Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

x. Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kungilia kazi kwa waajiri wao na waajiri wajiridhishe ipasavyo.

xi. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

xii. Waombaji wenye majina tofauti katika vyeti vya Taaluma, Kuzaliwa na NIDA waambatishe **DEED POLL.**

xiii. Waombaji wenye tofauti za herufi katika vyeti vya Taaluma, Kuzaliwa na NIDA waambatishe **Hati ya kiapo cha majina (Affidavit)**

xiv. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe **24.11.2025**.

xv. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili

**HAYATAFIKIRIWA.**

**MUHIMU**: Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliosainiwa pamoja na vyeti vya elimu kwenda kwa:

**Mkurugenzi wa Manispaa,**
**Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni,**
**S.L.P. 36009,**
**Kigamboni - Dar Es Salaam.**

*Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; https://portal.ajira.go.tz/ (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa* ***'Recruitment Portal').***

**Limetolewa Na: -**

**E. N. Kiwale**
**Mkurugenzi Manispaa ya Kigamboni.**